# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

*Simu:+ 255 282 250 1200*
*Nukushi:*
*Barua pepe: acl.mwanza@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Kamishna wa Ardhi Msaidizi,*
*Mkoa wa Mwanza,*
*S. L. P. 668,*
***Mwanza.***

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na. LD/LZ/ TIC/19** **24 Januari, 2025**

Meneja wa Kanda,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P 638,
**Mwanza.**

**YAH: KUWATAMBULISHA ENGLAND TECHNOLOGY CO. LIMITED WAMILIKI WA ARDHI ILIYOPO KIJIJI CHA NYASHINGWE, KATA YA CHABULA-WILAYA YA MAGU, MKOA WA MWANZA**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

**2.** Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi imepokea maombi ya kumilikishwa kiwanja/shamba/ardhi kutoka kwa Kampuni tajwa hapo juu. Kampuni hiyo inamilikiwa **ni watanzania.** Wamiliki wa kampuni hiyo walinunua ardhi hiyo yenye takribani **ekari 1.82** kutoka kwa wakazi wa asili wa eno hilo kama nyaraka zilivyo ambatishwa katika barua hii.

**3.** Aidha, Kampuni hiyo inatarajia kufanya uwekezaji wa kiwanda cha kutengeneza bidhaa za Plastiki lakini bado hawajapimiwa na kuandaliwa Hati Miliki katika ardhi hiyo. Uhakiki umefanyika uwandani hakuna mgogoro wa umiliki wa ardhi. Wamiliki wa eneo hili wamewasilisha maombi ya kuomba kupimiwa ardhi hiyo ili baadae waweze kuandaliwa Hati Miliki. Maelekezo ya utaratibu wa kufanya Upangaji, Upimaji na Umilikishwaji ardhi hiyo tayari yametolewa Kwenda Mamlaka husika (Halmashauri ya Wilaya ya Magu).

**4.** kwa barua hii, ofisi ya kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, inawatambulisha kwenu Kampuni hiyo kwa ajili ya kupatiwa cheti cha uwekezaji (***Certificate of Incentive***) kama wanavyo omba sambamba na taratibu nyingine zikiwa zinaendelea.

Nakutakia kazi njema,

Lucio A. Sambola
**Kny: Kamishna wa Ardhi Msaidizi**

KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI
S.L.P. 668, MWANZA

**Nakala:**

ENGLAND TECHNOLOGY CO. LIMITED,
S.L.P 10538,
**MWANZA.**

ENGLAND TECHNOLOGY CO. LIMITED,
S.L.P 10538,
**MWANZA.**

**Tarehe: 17 Januari, 2025**

Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
S.L.P 668,
**MWANZA**

**YAH: MAOMBI YA KUPIMIWA ARDHI KIJIJI CHA NYASHINGWE-WILAYA YA MAGU**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Sisi ni wamiliki wa ardhi iliyopo Kijiji cha Nyashingwe, kitongoji cha Nyamilama, kata ya Chabula-Wilaya ya Magu. Ardhi hiyo tumenunua kutoka kwa Bw. Amini Hussein Rukoba ambaye naye alinunua ardhi hiyo kutoka kwa wamiliki wa asili. Ardhi hiyo ina ukubwa wa ekari 1.82. Kampuni yetu ni kampuni ya Kitanzania.

Tunaomba kupitia ofisi yako ya Mkoa itusaidie Kupanga, Kupima na mwisho tumilikishwe ardhi hiyo ili tuweze kuiendeleza kwa mujibu wa Sheria. Kampuni yetu itagharamia shughuli hiyo ya Upangaji, Upimaji na Umilikishwaji (Hati Miliki). Pamoja na barua hii tunambatisha nakala za ununuzi ardhi pamoja na 'sketch' ya eneo hilo kwa urahisi wa rejea yako.

Tunatumaini kupata ushirikiano wa kutosha,

Kassim Mwita Mika (Mkurugenzi)..............................

Amini Hussein Rukoba (Mkurugenzi)..............................

ENGLAND TECHNOLOGY CO. LIMITED
18 DEC 2024
S.L.P. 10538
MWANZA

CamScanner

**MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA/KIWANJA.**

MKATABA huu umefanyika leo tarehe 15 mwezi 12 mwaka 2024.

KATI YA

**AMINI HUSSEIN RUKOBA, Mkazi wa ILEMELA wilaya ya ILEMELA mkoa wa MWANZA** (ambaye hapa atajulikana kama "MUUZAJI" pamoja na warithi wake) kwa upande mmoja wa mkataba huu.

NA

**ENGLAND TECHNOLOGY COMPANY LIMITED,** yenye Anuani 10538, Mwanza (ambaye hapa atajulikana kama "MNUNUZI") kwa upande mwingine.

KWAMBA Muuzaji ameonyesha nia ya kuuza SHAMBA/KIWANJA na mnunuzi amekubali kununua.

**BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

1. Kwamba Muuzaji na Mnunuzi tajwa hapo juu wote kwa pamoja wamekubaliana kuuziana SHAMBA/KIWANJA lililopo kijiji cha NYASHIGWE, kitongoji cha NYAMILAMA, kata ya CHABULA, wilaya ya MAGU mkoani MWANZA Shamba/kiwanja hilo lenye urefu wa miguu 105 na upana wa miguu 70 na ndani ya shamba/kiwanja hilo kuna MITI POLI shamba/kiwanja ambalo lilishalimwa.
2. KWAMBA muuzaji na mnunuzi wamekubaliana kuuziana shamba/kiwanja lenye MIPAKA Ifuatayo :
   i. Upande wa mashariki wa shamba/kiwanja hilo limepakana na **BARABARA YA MUSOMA**
   ii. Upande wa magharibi wa shamba/kiwanja hilo limepakana na **MZEE JAPHAT**
   iii. Upande wa kaskazini wa Shamba/kiwanja hilo limepakana na **AMINI HUSSEIN**
   iv. Upande wa kusini wa Shamba/kiwanja hilo limepakana na **BARABARA**
3. Kwamba Muuzaji kwa hiari yake mwenyewe amekubali kumuuzia Mnunuzi SHAMBA/KIWANJA lililoainishwa kwenye mkataba huu na Mnunuzi amekubali kununua SHAMBA/KIWANJA Husika bila ya kulazimishwa na mtu yeyote na mazingira yoyote.
4. Kwamba wahusika wa mkataba wamekubaliana kwa pamoja kuwa bei ya mauziano ya SHAMBA/KIWANJA Husika ni shilingi za kitanzania MILIONI ISHIRINI NA MOJA (21,000,000/)tu.
5. Imekubalika ya kwamba pesa tajwa kwenye aya ya nne (4) inalipwa kwa awamu moja siku ya kusaini mkataba huu.
6. Kwamba kwa kusaini mkataba huu Muuzaji anakiri kupokea pesa iliyotajwa kwenye aya ya nne (4) ya mkataba huu na Mnunuzi anakiri kumkabidhi Muuzaji kiasi hicho.
7. Imekubalika pia baada ya kusaini mkataba huu Mnunuzi atakuwa ndiye mmiliki halali wa SHAMBA/KIWANJA hilo lililoelezwa katika Mkataba huu.

CamScanner

8. KWAMBA endapo muuzaji atakuwa amefanya udanganyifu wa kuuza shamba/kiwanja ambalo sio mali yake hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
9. Kwamba Muuzaji anatamka bayana kwamba SHAMBA/KIWANJA halidaiwi na mtu yeyote na wala hakuna kesi yoyote iliyopo mahakamani au kwenye baraza lolote inayohusiana na miliki au mipaka ya SHAMBA/KIWANJA hilo. Na vile vile muuzaji anatamka bayana kwamba SHAMBA/KIWANJA hilo halijawekwa rehani au poni kama dhamana ya deni lolote lile analodaiwa Muuzaji au analodhamini.
10. Kwamba mkataba huu unatawaliwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KWA UTHIBITISHO WA MAKUBALIANO YALIYOAINISHWA KWENYE MKATABA HUU, WAHUSIKA WA MKATABA WAMEWEKA SAINI ZAO HAPA CHINI:**

Imesainiwa MWANZA **na ,**

**AMINI HUSSEIN RUKOBA**

Ambaye ni memfahamu kwangu binafsi. ..................

Leo tarehe 15 Mwezi 12 Mwaka 2024 MUUZAJI

MBELE YANGU

JINA: SALMA AMIN HUSSEIN

SAHIHI: ..............................

ANUANI: 32176 DAR ES SALAAM

CHEO: WAKILI

Salma Amin Hussein
Box 32176 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Imewekwa muhuri na kampuni

**ENGLAND TECHNOLOGY**

**COMPANY LIMITED** .......................... leo tarehe15 Mwezi12 Mwaka

2024 MNUNUZI

JINA: KASSIM MWITA MIKA

SAHIHI: ..............................

ANUANI: 10538 MWANZA

CHEO: DIRECTOR

ENGLAND TECHNOLOGY CO. LIMITED
15 DEC 2024
S.L.P. 10538
MWANZA

JINA: AMINI H. RUKOBA

SAHIHI: ..............................

ANUANI: 1103

CHEO: DIRECTOR